Imefadhiliwa na
Umoja wa Ulaya

# Boresha Chai - Kuboresha Mapato na Lishe ya Wakulima Wadogo wa Chai Kusini mwa Tanzania

1 NO POVERTY
2 ZERO HUNGER
5 GENDER EQUALITY
12 RESPONSIBLE CONSUMPTION AND PRODUCTION

**Boresha Chai inakuza vipato endelevu, lishe, na usawa wa kijinsia kati ya familia zinazolima chai kusini mwa Tanzania.**



## TAARIFA MUHIMU

**Sekta:** Chai
**Mshirika Kiongozi:** IDH the Sustainable Trade Initiative
**Washirika Wengine:** CEFA; Taasisi ya Utafiti wa Zao la Chai (TRIT), Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TSHTDA)
**Bajeti:** EUR 5 560 000
**Mchango wa EU:** EUR 5 000 000
**Muda wa Mradi:** 2020 - 2024



## USULI

Chai ni sekta yenye athari kubwa nchini Tanzania. Takriban jumla ya wakulima wadogo 31,000 wanazalisha theluthi moja ya pato la nchi. Zao la chai huvunwa mwaka mzima hivyo ni chanzo cha kutegemewa cha mapato kwa wakulima.

Walakini, sekta ya chai inakabiliwa na changamoto kubwa: wakulima wadogo wa chai nchini Tanzania hupata mavuno madogo. Hivyo, viwanda havipati majani mabichi ya chai yenye viwango na ubora unaotakiwa mara kwa mara ili kuviwezesha kuendesha biashara zao vizuri na kushusha gharama za uendeshaji. Hivyo, viwanda vinaishia kununua majani ya chai kwa bei ndogo kutoka kwa wakulima.

Kutokana na sababu hizi na zinginezo, ikiwemo kutomiliki au umiliki mdogo wa hisa katika viwanda vya usindikaji, wakulima wa chai nchini Tanzania hupata kiwango kidogo sana cha bei ya mnada wa Mombasa. Matokeo yake ni kwamba uzalishaji wa chai wa wakulima wadogo unashuka, na kusababisha wakulima wa Tanzania kuwa miongozi mwa wakulima wanaopokea kipato kidogo zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

**AGRI-CONNECT**

**Kusaidia Minyororo ya Thamani kwa Ustawi wa Pamoja katika Mazao ya Kahawa, Chai na Bustani**

## MAELEZO YA MRADI

1. Kuimarisha vyama vya ushirika vya wakulima wa chai ili:
   - Kutoa mafunzo
   - Kuhamasisha uongozi wa wanawake na ushiriki wa vijana katika vyama hivyo
   - Kutoa msaada wa kifedha kwa vyama kwa ushirika ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wanachama wao
2. Utoaji endelevu wa huduma, mafunzo na malipo yanayozingatia ubora wa mavuno kwa wakulima wadogo wa chai ili:
   - Kuanzisha Mifumo ya Utoaji wa Huduma Endelevu kwa vyama vya ushirika vya chai na wakulima
   - Kujenga uwezo wa wakulima wadogo wa chai kupitia Shamba Darasa
   - Kuweka mfumo wa malipo ya ziada ili kukuza na kutunza ubora wa juu zaidi wa majani mabichi ya chai
3. Ubunifu endelevu:
   - Kuonyesha na kukuza matumizi bora ya virutubisho katika mashamba madogo ya chai
   - Kuonyesha na kukuza huduma za uvunaji chai kwa kutumia mashine
   - Kuonyesha na kukuza umwagiliaji wa mashamba madogo ya chai
   - Kuanzisha vitalu vilivyoboreshwa vya vipandikizi kwa ajili ya kuongeza tija na uhimili wa mazao dhidi ya mabadiliko ya tabianchi
   - Kukuza huduma za kifedha na utoaji taarifa za kidijitali kwa wakulima wadogo wa chai
4. Uanuwaishaji wa mapato:
   - Hukusanya washirika kwa ajili ya huduma za shughuli za sekondari za mnyororo wa thamani na mauzo ya baadaye ya mavuno
   - Kutekeleza Mifano ya Utoaji wa Huduma Endelevu kwa shughuli za sekondari za mnyororo wa thamani na kuanzisha utafutaji na uunganisho katika masoko.
5. Lishe na uamuzi wa familia kwa kufanya yafuatayo:
   - Kukuza lishe bora katika familia kupitia uhamasishaji, mafunzo na uonyeshaji mifano.
   - Kujenga uelewa kuhusu masuala ya kifedha na kukuza uamuzi wenye usawa katika familia zinazolima chai.

## WASHIRIKA

Tea Research Institute Tanzania

the sustainable trade initiative

CEFA Il seme della solidarietà

## MATOKEO YATARAJIWAYO

Mradi unatarajia kufikia:

- Wakulima wadogo wa chai 22,000 – hii ni zaidi ya asilimia 70 ya wakulima wadogo wa chai wa Tanzania. Takriban wakulima 1,600 katika Wilaya ya Mufindi, 5,000 katika Wilaya ya Njombe, na 15,000 katika Wilaya za Rungwe na Busokelo
- Vyama vya ushirika 34 vya chai na / au vikundi vya wakulima
- Takriban wanachama 103,000 katika kaya zinazolima chai (wastani wa watu 4.7 katika kila kaya) Kampuni za chai za sekta binafsi zilizobanwa na kiwango cha chini na kisichokuwa na uthabiti wala ubora wa majani mabichi ya chai yanayovunwa na wakulima.

Ifikapo mwisho wa mradi, matokeo yafuatayo yanatarajiwa:

- Shamba Darasa 560 zimeanzishwa katika wilaya lengwa.
- Kuongezeka kwa mapato ya kaya kutokana na mavuno makubwa zaidi ya majani mabichi na mauzo kwa bei kubwa zaidi kulingana na ubora (ongezeko la asilima 50).
- Minyororo ya thamani minne isiyo ya chai imeimarishwa na asilimia 50 ya familia za wakulima wadogo wa chai kuinua mapato yao.
- Kuboresha lishe ili kupunguza udumavu (kupungua wa asilimia 40).
- Kuongezeka kwa usawa wa kijinsia katika kaya, mashamba na vyama vya ushirika (50% ya wanawake katika kaya ndogo za chai wanaoripoti kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na ufanyaji maamuzi). Kupunguza udhaifu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi (kutokana na kupanda aina ya chai inayohimili ukame, kutekeleza taratibu nzuri ya kilimo, kuwa na mfumo wa umwagiliaji, na uanuwaishaji wa mapato).
- Kuboresha uwezo wa shirika na utendaji wa vyama vyote 34 vya ushirika vya wakulima.
- Utoaji wa huduma mpya na ulioboreshwa kwa wanachama wa vyama vya ushirika visivyopungua 10. Kuongezeka kwa uanachama wa kamati, haswa wa wanawake na vijana (kuwe na wanawake 102 katika kamati za kijinsia na vijana 68 katika kamati za vijana katika ngazi ya ushirika).
- Kuongezeka kwa ubora na wingi wa majani mabichi ya chai yanayovunwa na wakulima wadogo kutoka 50% hadi 65%.

## MAWASILIANO

**IDH Tanzania**
Plot 38 Zone II, 51108 Gangilonga,
SLP 2458
Iringa, Tanzania
Barua Pepe: tarmahomed@idhtrade.org

Imefadhiliwa na Umoja wa Ulaya

Email: delegation-tanzania@eeas.europa.eu
https://www.eeas.europa.eu/delegations/tanzania

EuropeanUnionTanzania
EUinTZ